GAZETI LA MAENDELEO

Kiongozi : *Mutiri-wa-Bashara*

Mwaka wa 17 toleo la 398

Marais Buyoya, Habyarimana na Mobutu wajikamilisha



Ni katika mpango wa uhusiano wapaswa kuweko kati ya nchi tatu, ndugu, rafiki na jirani yaani Burundi, Rwanda na Zaïre, nchi hizo kaunda muungano wa kiuchumi «CEPGL». Maraïs mawaziri na wataalam kazaa wakutana mara kwa kutatua juu ya maswali yanayoweza kutia mkwazo kwa mwenendo bora wa siasa kaendeshwa. Kwa hiyo, kwa kukamilisha maoni na mahitaji yao kwa kudumisha uhusiano uliyoko, maraïs Buyoya, Habyarimana na Mobutu watezamiwa kukutana katika mkutano wa 12 wa kilele wa mjini wao Goma tarehe 30 hadi 31 mwezi huu wa January 1990.

Kuhusu mpango huo wa uhusiano mambo mengi yaliweza kuendeshwa barabara. Na kati ya hayo kusimikwa kwa miradi kazaa. Kati ya miradi hiyo yatezamiwa Benki ya maendeleo (BDEGL), shirika lenyi kuhusika na utafuti, kuhusu mlimo na ufugo wa wanyama (IRAZ) na ambalo jiwe la msinji wa vyumba vitakavyohusika na kazi latezamiwa mnamo tarehe 28 januari mjini Gitega (Burundi). Na mnamo tarehe 29 za mwezi huu, kuzinduliwa kiserkali kwa bwawa la moto wa stimu Ruzizi II jimboni mwa Kivu ya Kusini (Zaïre). Sherehe hizo zote zitaendeshwa mbele ya majumbe yatakayoongozwa na maraïs Buyoya, Habyarimana na Mobutu wa nchi-memba zà muungano wa kiuchumi wa nchi zinazopakana na maziwa makuu yaani Burundi, Rwanda na Zaïre.

Bwawa la Ruzizi II

Bwawa la moto wa stimu Ruzizi II kakamilisha utafuti wa majawabu yanayohitajika kwa kurahisisha maisha ya raïa wa nchi-memba za «CEPGL» kulingana na siasa kaendeshwa siku nenda rudi na maraïs wa nchi hizo.

Tukichungua vizuri, matukio ya kazi za bwawa hilo yatafikilia viwanda vingi kuundwa bali pia kazi za ujamii zitaweza kuendeshwa kama inavyohitajika kwa mfano kunako mahospitali, masomo na vituo vya upashaji wa habari. Isiweko hayo tu, bali pia kudumisha uhusiano na kutoa jimbo la Kivu ya zamani katika magumu-kazaa, hasa ya ununuzi, uchuuzi na usafirishaji wa bizaa.

Bwawa la moto ya stimu Ruzizi II lapatikana kunako kilometri 16 na mji wa Bukavu katika mkoa wa Mumosho, mtaani Kabare (Kivu ya Kusini).

Kazi za ujenzi wa bwawa hilo ziliendeshwa muda wa miezi 60 na wafanyakazi karibu 1000 wageni kama vile raïa chini ya uchunguzi wa shirika «COGEFAR». Kazi hizo ziligarimu kiasi cha dolari 93.038.000 za kiamerika kwa kuzitimiza.

Shirika SINELAC

Shirika SINELAC ndilo litahusika na kazi za ugawaji wa moto wa stimu ambao utafikia MW44 siku za usomi. Shirika hilo lina watumishi 102 kwa sasa kunako ofisi yake mjini Bukavu (Zaïre).

Viongozi wa shirika hilo ni Nyioni Bonaventure, kiongozi mkuu toka Rwanda, Mbesherubusa Déogratias, kiongozi ahusikae na ustadi, mwanachi Badiata Meeh, kiongozi ahusikae na feza. Na kunako baraza la uongozi, kuna washauri 6, kila nchi-memba kutoa watu ao wajumbe wawili. Burundi : Barandereka Bernard na Ndayizeyi Audance, Rwanda : Nsabimana Marcel na mwengine hajajulishwa bado, Zaïre : Mutamba Dibwe na Mbuze.

Itajulishwa hapa kuwa ni mashirika SNEL (Zaïre), ELECTROGAZ (Rwanda) na REGIDESO (Burundi) ndiyo yatahusika na ugawaji wa moto huo wa stimu nchinimemba baada ya kuukabiziwa na shirika SINELAC.

BISIMWA L.B. TSEROU

Uhariri

UTASHI BORA

Muungano wa kiuchumi wa nchi zinazopakana na maziwa makuu (CEPGL) ambao kaundwa mnamo tarehe 20 septemba 1976 na kufikilia hapo makesho miaka 14, ingawa muda huo si mrefu, kulingana na ukomo wake, waonya siku kwa siku utashi bora wa maraïs Buyoya wa Burundi, Habyarimana wa Rwanda na Mobutu wa Zaïre kwa kufikilia mahitaji ya uhusiano bora kati ya nchi zao.

Kwa kweli kazi za kuhimiza nchi-memba za Muungano huo kwa kufikilia ukomo wa siasa ya kiuchumi wa kweli kati ya nchi hizo sio mzaa. Yafaa kupinga magumu yote yanayoweza kutukia tukitegemea uhuru wa nchi na utashi wa kujiokoa.

Ingawa magumu hayo ambayo yatalazwa siku kwa siku, «CEPGL» imekwisha twika misinji ya maendeleo ya nchimemba. Kwa mfano amani na usalama, misinji yenyewe ya siasa bora ya kiuchumi, yatezamiwa nchini-memba na kati yazo, kuundwa kwa mashirika majuzi na ya kipekee ya muungano wa kiuchumi «CEPGL» ili kutafuta majawabu kwa maswali yaliyoko kuhusu maendeleo hasa katika mlimo na vyakula, nguvu za umeme na zinginezo, pia toleo la feza kwa uendeshaji wa miradi.

Mambo yaliyokwisha kutimizwa kama vile ujenzi wa bwawa wa Ruzizi II kwa moto wa stimu, pia hayo yanayoendeshwa kwa kutimiza kazi zinazohitajika kwa udumisho wa muungano huo wa kiuchumi yaonya kuwa nchi-memba zakubali kweli kuungana mkono kwa kuzipatia hali bora ya maendeleo na hiyo itawezekana kutokana na miungano ya kiuchumi.

Kuundwa kwa muungano wa kiuchumi wa nchi za Burundi, Rwanda na Zaïre (CEPGL) haitupilie mbali mengineo miungano. Maendeleo yao ni kwa manufaa ya wote. Ushirika wa nchi-memba wategamia historia, mazingira, utamaduni na ukoo wa raia wa nchi-memba na mambo ambayo ni msinji wa kuundwa wa miungano iliwaruhusu kufikilia matukio mara na mara magumu. Miungano hiyo yapaswa kuhimizwa na kuungwa mkono kabisa kwa kuwa msinji wa kweli na mguu ambao utaweza kuwa nguzo ya soko moja kuu la kiafrika.

Isiwe tu mradi ila ujio bora ambao [illegible] Burundi, Rwanda na Zaïre ambazo baada ya kuunda muungano wa kiuchumi wa nchi zinazopakana na maziwa makuu (CEPGL) zakamilisha shuruli lao kuhusu swali la kuunda muungano mkuu wa kiuchumi Barani Afrika na hiyo kutokana na utashi pia ujuzi bora wa maraïs watatu wa nchi-memba.

BABA WA TAIFA AZUNGUMZA NA RAIA KIDEMOKRASIA

Muda wa siku tatu, tangu tarehe 30 januari hadi 1 februari 1990, Baba wa Taifa, Mareshali Mobutu alistarehe na raïa jimboni mwa Kivu ya Kusini katika ziara ya kiserkali mjini Bukavu ambako kapokelewa na kusindikizwa kwa shangwe na vigelegele baada ya kuyatembelea majimbo ya Kivu ya Kaskazini na mbele ya kujielekeza mjini Kindu, jimboni Maniema. Na hiyo kisha miaka 6 sasa.

Jimboni mwa Kivu ya Kusini hapa mjini Bukavu, Prezidenti-Muundaji wa Chama cha Mapinduzi, akiwa na shuruli ya kujionea binafsi mambo yaliyoko, alitembea mitaani kisirisiri na kuwapokea katika masimulizi viongozi wa vikundi vya msinji mbalimbali ambao waliweza kumtoléa Mareshali matatizo mengi ambayo yakwamisha kweli maendeleo bora nchini. Ni hivi Raïsi Mobutu kasikia malalamiko ya wananchi, arkiaskofu wa dini katolika Mulindwa ambaye kamueleza juu ya maendeleo ya vyuo vikuu jimboni, bikira Muzigwa wa shule sekondari ya Nyakavogo ambaye kapewa msaada wa feza na vifaa kwa maelimisho ya wanafunzi, Kaboyi na Birindwa, wafanyabiashara ambao kamueleza Mareshali Mobutu magumu na hasara yapatikanayo kwa usafirishaji wa watu na wa bizaa yao toka ubovu wa mabarabara, mama Kabare katoa maoni yake kuhusu masikilizano na uongozi kiasili katika mikoa, Mutiri-wa-Bashara, kiongozi-mhariri wa gazeti JUA na mwenyekiti wa muungano wa viongozi-wahariri wa magazeti nchini, ambaye kamuonya mheshimiwa Mobutu magumu ya waandishi na wapashahabari hukuta kwa kuendesha bora kazi zao za uhimizaji nchini. Si hayo tu, kwani Baba wa Taifa kawapokea wengine viongozi na wakuu madarajani kote na kamkabizi mwanchi Mokolo wa MPombo, kiongozi wa ofisi ihusikayo na kusikia pia kukusanya maoni, malalamiko na mashauri ya watu, kusikia na kuchungua kwa karibu mambo hayo.

Itakumbushwa hapa kwamba Raïs Mobutu kahuzunika kutambua mji mzuri kama Bukavu hapo zamani, leo hii walazwa usiku katika giza mahali mengi. Pia Baba wa Taifa kasimamia mkutano wa kwanza wa Baraza la mawaziri mwezini huu februari mjini Goma siku ya tano tarehe 2. Baada ya wanamemba wa Baraza hilo kukutana mjini Kindu Maniema mwisho wa mwezi wa januari chini ya uongozi wa waziri mkuu Kengo wa Dondo.

Bisimwa L.B. Tserou